



ELLEN WHITE PRE AND PRIMARY SCHOOL

P. O. Box 3118, Nzuguni Dodoma – Tanzania

Mob: 0769 352 215 / 0673 443 962

Email: info@ews.sc.tz Web: www.ews.sc.tz

NAFASI ZA AJIRA

18/12/2024

Utangulizi

Ofisi ya Meneja wa shule ya **Ellen White School- Dodoma**, inapenda kuutangazia umma kuwa shule imetoa nafasi mbalimbali za ajira kama ifuatavyo:-

1. Walimu Nafasi 15

Waajiriwa katika nafasi wanatakiwa kuwa wenye sifa zifuatazo:-

- I. Wenye Astashahada (Cheti), Stashahada (Diploma) au Shahada ya ualimu wa elimu ya msingi au elimu ya awali (**Early Childhood Education**)
- II. Wenye Stashahada au Shahada ya ualimu wa Michezo, Muziki, Tehama (ICT), Kichina, Kifaransa na Dini

2. Dereva (Drivers II) Nafasi 5

Waajiriwa katika nafasi hii wanatakiwa kuwa wenye sifa zifuatazo:-

- I. Wenye cheti cha Darasa la saba au kidato cha nne (Form IV) na leseni Daraja C2, C1 na C ya uendeshaji magari ambayo imefanyiwa kazi kwa muda usiopungua miaka miwili bila kusababisha ajali.
- II. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo VETA/NIT au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- III. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

3. Wapishi Nafasi 2

Waajiriwa katika nafasi hii wanatakiwa kuwa wenye sifa zifuatazo:-

- I. Awe amemaliza darasa la saba au kidato cha nne.
- II. Awe amefanya kazi ya kupika kwa muda usiopungua miaka miwili.
- III. Awe anajua hesabu na vipimo vya chakula.
- IV. Awe anajua kupika vizuri mapishi ya aina zote
- V. Awe anajua kuandaa bajeti ya chakula
- VI. Awe na nidhamu kwenye kazi na lugha nzuri kwa watumishi na wanafunzi
- VII. Awe anatambua suala la usafi na ajue kuzingatia muda wa kula
- VIII. Awe mbunifu katika upishi na uwezo wa kujifunza kutoka kwa wengine.

4. Walezi wa watoto (Matrons) Nafasi 3

Waajiriwa katika nafasi hii wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

- I. Wenye elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- II. Wenye uwezo wa kuongea na kusoma lugha ya kiingereza kwa ufasaha
- III. Wenye elimu katika fani ya ualimu, uuguzi na ustawi wa jamii watafikiriwa kwanza.
- IV. Wenye uzoefu na kazi hii usiyopungua miaka mitatu
- V. Wenye umri kuanzia miaka 30 na usiozidi miaka 50.
- VI. Wenye maadili mema na wacha Mungu.

5. Mhasibu Nafasi 2

Waajiriwa katika nafasi hii wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

- I. Wenye elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- II. Wenye Stashahada au Shahada ya uhasibu kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.
- III. Wenye uzoefu na umahiri wa kufunga hesabu kwa muda usiyopungua miaka mitatu

Masharti ya jumla kwa kazi zote

- I. Waombaji wote waambatanishe maombi yao na vivuli vya cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha NIDA.
- II. Waombaji waambatanishe maelezo yao binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani, namba ya simu ya kuaminika, pamoja na majina matatu ya wadhamini wa kuaminika.
- III. Maombi yote yaambatane na vivuli vya vyeti vya taaluma (kidato cha nne, sita nk.) pamoja na picha moja ya passport iliyopigwa hivi karibuni.
- IV. Waombaji wote wawe na uwezo wa kuongea, kusoma na kuandika lugha ya kingereza
- V. Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kingereza/Kiswahili.

Zingatia

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na zitumwe kwenye barua pepe info@ews.sc.tz au anwani tajwa hapa chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05/01/2025 muda wa saa za kazi.

**SCHOOL MANAGER
ELLEN WHITE SCHOOL
P.O BOX 3118
DODOMA**